University of Dar es Salaam

Library Repository **https://libraryrepository.udsm.ac.tz**

Mwalimu J.K Nyerere Books about and by Mwalimu Nyerere

1967

Uhuru na maendeleo

Nyerere, Julius Kambarage

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Nyerere,J.k(1967).Uhuru na maendeleo. Dar es Salaam:Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,p.14
http://41.86.178.5:8080/xmlui/handle/123456789/7158
Downloaded from University of Dar es Salaam Library Repository

UHURU NA MAENDELEO

Julius K. Nyerere

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

Bei Shs. 1/50

500/=

UHURU NA MAENDELEO

Julius K. Nyerere

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania

UHURU NA MAENDELEO

Uhuru na Maendeleo ni vitu vinavyohusiana sana; uhusiano wao ni sawa na uhusiano baina ya kuku na yai! Bila ya kuku hupati mayai; na bila mayai kuku watakwisha. Vile vile, bila ya uhuru hupati maendeleo, na bila ya maendeleo ni dhahiri kwamba uhuru wako utapotea.

Uhuru unategemea maendeleo

Tunapozungumza habari za uhuru maana yetu nini hasa? Kwanza, kuna uhuru wa nchi; yaani uwezo wa wananchi wa Tanzania kujipangia maisha yao, wakijitawala wenyewe bila ya kuingiliwa kati na mtu ye yote asiyekuwa Mtanzania. Pili, kuna uhuru wa kutosumbuliwa na njaa, maradhi na umasikini. Na tatu, kuna uhuru wa mtu binafsi; yaani haki yake ya kuishi, akiheshimika sawa na wengine wote, uhuru wake wa kusema, na uhuru wake wa kushiriki katika uamuzi wa mambo yote yanayogusa maisha yake, na uhuru wa kutokamatwa ovyo na kutiwa ndani kwa kuwa tu kamuudhi mkubwa, japo kama hakuvunja sheria yo yote. Yote hayo ni mambo yanayohusu uhuru, na hatuwezi kusema kuwa Wananchi wa Tanzania ni huru, mpaka tuwe tuna hakika kwamba wanao uhuru wa mambo yote hayo.,

Lakini ni dhahiri kwamba mambo hayo yanategemea maendeleo ya uchumi. Madhali nchi yetu bado masikini, na wananchi hawakupata elimu, na ni wajinga na wanyonge, basi uhuru wetu wa kujitawala unaweza kuhatarishwa na taifa lo lote la kigeni lenye maendeleo na nguvu zaidi. Maana kama ni lazima kununua silaha, gharama za silaha hizo zitatoka katika uchumi wa nchi. Lakini hili si jambo la silaha peke yake, ni

jambo linalohusu wananchi wa taifa kutambua kwamba wao ni watu huru na uhuru huo wanapaswa kuulinda, kama ulinzi huo ni wa silaha au kama ni wa njia nyinginezo.

Ni dhahiri vile vile kwamba uhuru wa kutosumbuliwa na njaa, maradhi na umaskini unategemea maongezeko ya mali na elimu nchini : maana watu wanaweza tu kutumia mali waliyo-ichuma. Na hata uhuru wa mtu binafsi utakuwa na maana kama shabaha yake ni maendeleo. Mtu anaweza kutetea haki zake barabara kama haki hizo anazijua, na anajua jinsi ya kutumia njia za Katiba iliyopo kutetea haki hizo. Hata ujuzi wa namna hiyo ni maendeleo.

Maana ukweli ni kwamba maendeleo maana yake ni maendeleo ya **watu.** Mabarabara, majumba, kuongeza mazao, na vitu vingine vya aina hii, siyo maendeleo : ni vyombo vya maendeleo. Barabara mpya inampanulia mtu uhuru wake kama anaitumia kwa kusafiri. Kuongeza idadi ya majengo ya shule ni maendeleo kama majengo hayo yanaweza kutumika, na yana-tumika, kuongeza ujuzi na elimu ya watu. Kuongezeka kwa mazao ya ngano, mahindi na maharage ni maendeleo ikiwa tu watu watapata chakula bora zaidi. Kuongezwa kwa mazao ya pamba, kahawa au mkonge ni maendeleo kama mazao hayo yanaweza kuuzwa, na fedha zikatumika kwa kununulia vitu vingine vitaka-vyowawezesha watu kuwa na afya bora zaidi, starehe zaidi, na elimu zaidi. Maendeleo yasiyokuwa maendeleo ya watu yana-weza yakawapendeza wataalam wa historia wa mwaka 3000; lakini kwetu sisi hayana maana kwani hayahusiani na maisha ya kesho tunayoyajenga. Kwa ajili hiyo, kwa mfano mapiramidi ya Misri, na mabarabara ya Warumi yaliyoko Ulaya yalikuwa maendeleo ya vitu ambavyo mpaka leo yanatushangaza. Lakini kwa kuwa yalikuwa majengo tu, na watu wa wakati huo hawa-kuendelea, basi dola na utamaduni wake vimeteketea zamani sana. Utamaduni wa Misri wa wakati huo ijapo ulikuwa na busara na elimu nyingi, haukukawia kuteketezwa na wageni, maana ulikuwa utamaduni wa wachache : wananchi waliobaki walikuwa watumwa walioteseka tu kwa shughuli za kuleta maendeleo ya majengo, ambayo wao wenyewe hawakuyatumia

Kadhalika, dola ya Warumi iliposhambuliwa, na majeshi yake yakakimbilia kwao, yale mabarabara mazuri na majengo

yaliyokuwako yalioza tu, kwa sababu hayakuwa na maana kwa wale waliokaa sehemu zile. Zaidi ya hayo, haiyumkini kwamba kuwapo kwa mapiramidi au kwa mabarabara ya Warumi kumeongeza lo lote katika historia ya nchi zinazohusika, au ya maisha ya wananchi wa humo.

Maendeleo huzaa uhuru, ikiwa maendeleo yenyewe ni maendeleo ya watu. Lakini watu hawaendelezwi; ila watu hujiendeleza wao wenyewe. Ingawa inawezekana mtu mmoja kumjengea nyumba mtu mwingine; haiwezekani hata kidogo mtu mmoja kumfanya mwingine ajivune au ajiamini kuwa sawa na binadamu wengine. Hayo ni mambo ambayo hayana buni yatokane na mtu mwenyewe na kwa vitendo vyake mwenyewe. Anajiendeleza mwenyewe kwa vitendo atendavyo; anajiendeleza kwa kujiamulia mambo yake mwenyewe; kwa kuongeza ujuzi na uwezo wake mwenyewe na kwa kushirikiana akiwa mtu sawa na wenzake kujenga maisha ya kijiji anamoishi. Hivyo, kwa mfano, mtu anajiendeleza mwenyewe wakati akilima mazao ya kutosha, au akipata fedha za kutosha, kujiletea maisha bora yeye na jamaa yake. Haletewi maendeleo kama mtu mwingine akimpa vitu hivyo. Mtu anajiendeleza mwenyewe kama akijiongezea elimu yake katika jambo lo lote; lakini haletewi maendeleo kama anatenda mambo anayoamriwa na mtu mwingine mwenye elimu zaidi bila ya kuelewa amri hizo zinazotolewa kwa sababu gani. Mtu anajiendeleza akijadiliana na wenziwe kuhusu mpango mpya, na hatimaye akashiriki katika uamuzi wake; haletewi maendeleo kama akiswagwa kama mnyama kutimiza mpango mpya asiouelewa. Kwa kweli maendeleo ya binadamu yanaweza kuletwa na mwanadamu mwenyewe; maendeleo ya watu yanaweza kuletwa na watu.

Mwisho, kama maendeleo yanaongeza uhuru wa watu, basi lazima yawe maendeleo yanayowafaidia watu. Lazima maendeleo hayo yawe na faida kwao, na kumaliza shida zao. Kila mpango uamuliwe kwa kupima kama unatimiza shabaha ya maendeleo, na shabaha ya maendeleo ni watu. Lakini kama mpango unasaidia maendeleo ya watu na kama unatimizwa na watu kwa hiyari yao, mpango huo utatimiza haja za watu, mradi masharti matatu yametimizwa. Kwanza, kama watu wanaelewa shida zao. Pili, kama wanaelewa jinsi shida hizo zinavyoweza kumalizwa. Na tatu, kama wana uhuru wa kujiamulia mipango yao, na kuitimiza

Maendeleo yanategemea uhuru

Kama shabaha ya maendeleo ni kuongeza uhuru na maisha bora ya wananchi, shabaha hiyo haiwezi kutimizwa kwa nguvu. Iko methali inayoeleza ukweli wa jambo hili. Punda unaweza kumlazimisha kwenda kisimani; lakini huwezi kumlazimisha kuyanywa maji. Kwa amri, au kwa utumwa, unaweza kujenga mapiramidi na mabarabara makubwa makubwa; unaweza kupanua mashamba, au ukaongeza idadi ya vitu vinavyotengenezwa viwandani mwako. Vitu vyote hivi, na zaidi vinaweza kupatikana kwa kutumia nguvu; lakinni havileti maendeleo ya watu. Utumiaji wa nguvu, na kutoa ahadi za uwongo, mambo hayo yanaweza kuleta mafanikio kwa muda mfupi tu. Hayawezi kuleta nguvu kwa taifa au kijiji, wala hayawezi kuweka msingi wa uhuru wa watu, au usalama wa mtu binafsi au wa kikundi cha watu.

Kuna njia moja tu unayoweza kutumia kuwafanya watu wajiletee maendeleo yao wenyewe. Njia yenyewe ni kwa kuwaeleza na kuwaongoza. Kwa njia hizo, na njia hizo peke yake, watu wanaweza kusaidiwa wakaelewa shida zao na mambo yanayoweza kufanya kumaliza shida hizo. Huu ndiyo uongozi unaopaswa kutolewa na viongozi wa TANU na wa Serikali; hii ndiyo njia ya kuleta maendeleo katika Tanzania. Lakini, ingawa tunapaswa kutoa uongozi wa namna hiyo, uamuzi lazima utoke kwa watu wenyewe, na wao wenyewe lazima waitimize mipango waliyoamua.

Kwa hiyo kuna mambo muhimu mawili katika maendeleo ya watu. La kwanza ni uongozi wa kueleza, na pili demokrasi katika kuamua mambo. Maana uongozi maana yake siyo kuwakemea watu; maana yake siyo kuwatukana watu au kikundi cha watu usiokubaliana nao; wala maana yake siyo kuwaamuru watu kutenda hili au lile. Uongozi maana yake ni kuzungumza na kushauriana na watu, ukiwaeleza na kuwashawishi. Maana yake ni kutoa mapendekezo yenye manufaa, kufanya kazi na watu, ukiwaonyesha, kwa vitendo, jambo unalowashauri kutenda. Maana yake ni kuwa mmoja wao, na kutambua kwamba wao ni sawa na wewe.

Na hususa, wakati huu wa historia yetu tusijaribu kuwalaumu watu au vikundi vya watu kwa mambo ambayo sisi binafsi hatuyapendi, au ambayo watu hawayapendi. Wanyonyaji ambao siku hizi wanaonekana wanapendwa sana na viongozi wetu hata wanawazungumza usiku na mchana, ni kipingamizi kidogo sana cha maendeleo yetu ya sasa. Wale wachache waliobakia wanaweza kumalizwa vema zaidi kama watu na viongozi wao watashikilia kutimiza kazi za maendeleo. Ni upuuzi kama sisi viongozi tutatumia muda wetu wote kuwatukana wanyonyaji — hasa kwa kuwa baadhi yetu hatufahamu kazi inayotendwa na baadhi ya hao tunaowatukana. Badala yake tungepaswa kutoa uongozi wenye mawazo mapya na wa maendeleo. Tungepaswa kujihimiza kuelewa mipango ya maendeleo ambayo TANU inajaribu kuelekeza, na tungeeleza mipango hiyo kwa watu. Tutakapokuwa tumewaridhisha watu kuwa mipango ya TANU ni mizuri na ya maana, basi tufanye kazi pamoja nao kuunda vijiji ambamo wanyonyaji hawatapata nafasi kufanya uovu wao.

Lakini kutoa uongozi maana yake siyo kuwanyang'anya watu wenyewe mamlaka yao. Watu lazima wafanye uamuzi wao wenyewe kuhusu maisha yao ya baadaye kwa kufuata njia za kidemokrasi. Uongozi hauwezi kuchukua nafasi ya demokrasi; uongozi lazima uwe sehemu ya demokrasi. Kama uamuzi utahusu mambo ya taifa zima, basi watu watafanya uamuzi huo kupitia Halmashauri Kuu ya TANU, au Mkutano wa Mwaka wa TANU, au kupitia Bunge. Kama jambo lenyewe linahusu Wilaya, basi watu watafanya uamuzi wao kupitia Halmashauri za Wilaya. Kama ni jambo la kijiji, kwa mfano kufanya kazi za kujitolea, basi wale wanaohusika ndiyo wanaopaswa kuamua, baada ya majadiliano. Hakuna njia nyingine itakayoleta maendeleo. Maana, kama vile ambavyo watu hawapati uhuru kamili bila ya maendeleo, basi maendeleo halisi ya watu hayaji bila uhuru.

Mambo mawili ya lazima katika demokrasi

Lakini kuna mambo mawili ya lazima katika demokrasi; ukiyakosa hayo demokrasi hakuna. La kwanza ni kwamba kila mtu lazima aweze kusema kwa uhuru kabisa,. na maneno ya kila mtu lazima yasikilizwe. Hata kama mawazo ya mtu huyu hayapendwi kiasi gani, au walio wengi wanamdhania amepotoka kiasi gani, si kitu. Kama mtu anapendwa kwa wema wake, au

hapendwi kwa visa vyake, hayo yote si kitu. Kila Mtanzania, kila mtu kijijini, kila mjumbe wa Halmashauri ya Wilaya, kila Mbunge, n.k., lazima aweze kusema kwa uhuru bila hofu ya vitisho — ama katika mkutano ama nje ya mkutano. Watu wenye mawazo tofauti, hata wakiwa wachache, lazima wawe na haki ya kutoa mawazo yao katika majadiliano bila ya hofu ya kusumbuliwa; mawazo yao na yashindwe katika hoja za majadiliano, siyo kwa vitisho au mabavu. Majadiliano yenyewe yatakayoleta uamuzi lazima yawape nafasi watu kusema kwa uhuru kabisa. Na hata baada ya kuamua jambo watu wawe na uhuru kuendelea kulizungumza jambo hilo. Maana wale wachache wenye mawazo tofauti lazima wafahamu kuwa kama wanayo mawazo yenye maana, na kama wakiyaeleza mawazo hayo vizuri, wanaweza kubadili mawazo ya wale wengine walio wengi. Kadhalika wale walio wengi lazima wawe tayari kuyashikilia mawazo yao mpaka wale wachache waridhike kuwa uamuzi uliofanywa juu ya jambo lile ulikuwa sawa. Majadiliano lazima yaruhusiwe kuendelea, kwa uhuru kabisa. Hiyo ni sehemu ya maana ya uhuru wa mtu binafsi.

Lakini ile lazima ya kuwa na uhuru wa mazungumzo haiwezi kuruhusiwa kuzuia uamuzi kufanywa. Kuna wakati utafika mazungumzo yakatike na kitendo kifuate, ama sivyo hatutafanya kazi yo yote ila kubwata tu. Kama jambo limejadiliwa vya kutosha, na kila wazo limekwisha kutolewa, basi uamuzi lazima ufanywe, na hapo mawazo ya wengi lazima yaheshimike. Maana kama vile walio wachache walivyo na haki ya kusikilizwa, walio wengi wanayo haki ya kufuatwa. Uamuzi ukiisha fanywa, lazima ukubalike kuwa ni uamuzi wa watu wote; na wote, hata wale waliokuwa wakipinga, hawana budi kushiriki katika kutimiza jambo lile. Kwa hiyo, jambo la pili la lazima katika demokrasi ni kwamba sheria ikisha pitishwa lazima kila mmoja atii sheria ile, pamoja na wale walioipinga na wasiotosheka na hoja zilizotolewa kutetea sheria ile. Isitoshe, mara sheria ikipitishwa kuikubali peke yake hakutoshi, lazima kila mtu aitetee. Haitoshi mwananchi kuacha kuiba; lazima pia ashirikiane na polisi katika kuitimiza sheria, na lazima awapeleke polisi wale wanaoivunja sheria.

Maana lazima uweko utaratibu wa kutimiza uamuzi wa kidemokrasi. Walio wachache lazima waruhusiwe kutetea

mabadiliko katika sheria au katika uamuzi. Lakini kwa sasa lazima waitii sheria iliyopo, mpaka hapo watakapofaulu kuwashawishi walio wengi kukubali mabadiliko hayo. Bila ya utaratibu wa namna hiyo maendeleo ya aina yo yote hayawezekani. Wengi husikiliza maoni ya wachache na wachache kutii uamuzi wa wengi ndizo kanuni mbili kubwa za demokrasi.

Baada ya uamuzi utii

Lazima pawepo utii na utaratibu katika mambo yote ya maisha yetu. Na hauna budi uwe ni utii unaokinai; yaani unakubalika kwa hiari; maana ni sehemu muhimu ya uhuru na maendeleo. Uhuru mkubwa zaidi uanopatikana kwa watu kufanya kazi pamoja, na kuweza kuleta mafanikio makubwa kwa ushirikiano ambayo kila mmoja wetu peke yake asingeweza kuyapata, yote hayawezekani bila ya kufuata utii na utaratibu wa kutimiza uamuzi uliokubaliwa. Na hii maana yake ni kukubali mamlaka yaliyowekwa kisheria. Yaani kama tunafanya kazi kiwandani lazima tuukubali utaratibu wa kiwandani. Haidhuru kama kiwanda hicho ni cha umma ama ni cha bepari; sheria zake lazima zizingatiwe, na wakuu wa kazi hizo lazima tuwatii. Vivyo hivyo katika hospitali, katika mashule, ofisini na kadhalika. Kama daktari amemwandikia dawa mgonjwa, basi muuguzaji lazima aitoe dawa hiyo bila ulalamishi, na bila uzembe. Kama mwangalizi wa hospitali ameweka sheria kwa shabaha ya kuendesha kazi za hospitali vizuri, basi kila muuguzi sharti azifuatae sheria hizo. Kama kuna vipingamizi vinaweza kuelezwa, lakini kwanza utaratibu wa hospitali lazima ufuatwe, na yule asiyefuata akubali kufukuzwa. Na vivyo hivyo ndivyo inavyopaswa iwe vijijini mwetu. Kama kijiji kimejiamulia kidemokrasi kutimiza mpango fulani kwa njia ya kujitegemea, basi kila mmoja lazima ashiriki katika kuutimiza uamuzi huo, la sivyo akubali kupata adhabu itakayokuwa imepangwa na wananchi wa kijiji hicho.

Kwa kweli ikiwa uamuzi huo umefanywa kwa kibali cha walio wengi baada ya majadiliano yaliyoendeshwa kidugu, si vigumu kupata utii wa kutekeleza, na mara nyingi utii huu utakuwa wa hiari. Maana kama wananchi wanataka uhuru wao binafsi, na kama wanataka maendeleo, basi watakubali kuwa iko haja ya kufanya kazi kwa utii na utaratibu. Na kwa kweli

katika nchi yetu shida ya utii inaweza ikatokea tu ikiwa wananchi wenyewe hawaelewi maana ya mabadiliko tuliyokwisha kuyaleta katika maisha yetu. Katika maisha yetu ya Kiafrika ya asili tulikuwa na utii — mara nyingi amri zake zilikuwa kali. Kila mtu alizikubali sheria hizo, na kila mtu akashiriki katika kuzitimiza. Shida yetu sasa haitokani na utii wenyewe. Shida yetu ni kwamba hatuelewi utii na utaratibu ulio wa lazima wa kutimiza sheria katika taifa la kisasa; tunashindwa kuelewa aina mbali mbali za utii na utaratibu unaotakiwa katika kuendesha kijiji cha kisasa. Kwa mfano wakati ule ambapo kila kijiji kilipokuwa kikiangalia usalama wake, wezi waliadhibiwa huko huko vijijini. Lakini sasa ni lazima tukimwona mtu tunayemshuku kuwa ni mwizi tumpeleke polisi; watu wenyewe hawaruhusiwi kumpiga au kumtesa. Au vile vile sheria za kuendesha kijiji kilicho maporini peke yake hazifai kuendesha kiwanda cha kisasa. Huko kijijini mtu ana hiyari yake ya kufanya kazi; anaweza kuifanya alfajiri au adhuhuri. Lakini kiwandani, kama mtu mmoja hakufanya kazi yake katika wakati unaotakiwa, mamia ya watu wengine wanaweza kulazimika kukaa bure na kupoteza wakati wao.

Aina mpya hizi za utii na utaratibu lazima zikubaliwe na wananchi pamoja na viongozi wetu wote. Na kama yuko mtu asiyekubali wajibu wake katika jambo hili, basi hana budi akubali adhabu ya kushindwa kwake. Kama anavunja sheria, ataadhibiwa mahakamani. Kama anashindwa kufuata utaratibu wa kazi zake, basi lazima afukuzwe. Maana lazima tukubali kuwa watu wenye madaraka katika Tanzania hii sasa wanaifanya kazi hiyo kwa niaba ya wananchi wa Tanzania. Kama wakiifanya kazi yao vibaya, au kama wakishindwa kuheshimu ubinadamu wa kila mtu, basi TANU au Serikali itawaondoa katika uongozi au kazini na kuwatia wengine. Au wakati wa uchaguzi hawana budi waondolewe na wananchi. Lakini kwa wakati huu lazima watetewe ikiwa wanatekeleza sheria au wanatoa amri zinazokubaliwa na sheria. Hatuna budi kuacha kuwatukana watu wanaojaribu kutimiza sheria; tusimwite mtu mkoloni anaposhikilia kwamba watu lazima wafuate sheria za ofisi, au kiwanda, au hospitali, au shule, au mahali pengine po pote.

Kama tunataka maisha yetu yawe na amani na raha, na kama tunataka kufanikiwa katika shabaha zetu za kuinua maisha

yetu, basi lazima tuwe na uhuru pamoja na utii. Maana uhuru bila utii ni wazimu; na utii bila uhuru ni utumwa.

Lakini utii ni njia tu ya kutimiza uamuzi. Tunapodai utii katika mazungumzo ni kwa sababu ya kusaidia mazungumzo yaendeshwe vizuri na kwa utaratibu. Utii tunaousema hapa na kushurutisha ni mambo mawili mbali mbali. Wakati wa majadiliano ni lazima kufuata utaratibu ili kupata uamuzi. Kama tunataka kila mtu apate nafasi ya kusikilizwa, basi lazima uweko utii na utaratibu. Lakini mkutano ambao kila mtu anakubali tu kila wazo linalotolewa si mkutano wenye utaratibu. Mkutano wenye utaratibu ni ule ambao sheria za mkutano zilizokubaliwa kuwa ni za haki zinafuatwa na kila mmoja kwa hiyari. Kwa mfano kila mtu anasema kwa ruhusa ya Mwenyekiti; na kila mtu anaruhusiwa kutoa mawazo yake bila ya kuzomewa au kutukanwa. Maana utaratibu ndio unaofanya mambo yakaenda vizuri; ndiyo njia ya kutimiza uamuzi. Siyo njia ya kuufanya uamuzi wenyewe.

Vijiji vya Ujamaa

Ni jambo la maana kwetu kuelewa uhusiano baina ya uhuru, maendeleo, na utii, maana siasa yetu ya kujenga vijiji vya Ujamaa nchini kote inategemea mambo hayo. Maana kwa muda mrefu sasa tumefahamu kuwa maendeleo lazima yaende vijijini, na jambo hilo linataka kazi za ushirikiano wa watu wenyewe. Kwa hiyo tokea mwaka 1959 TANU imewashawishi watu wajiunge walime mashamba ya pamoja vijijini, na Serikali yetu ya TANU imeamrisha makazi mapya ya aina nyingi. Lakini sasa tunaweza kuona kwamba tumefanya makosa mengine, na ni jambo muhimu kwetu kujifunza kutokana na makosa hayo.

Hapo mwanzo tulipojaribu kuleta maendeleo ya vijijini wakati mwingine tulitumia fedha nyingi sana kujenga makazi mapya, kununua vifaa vya kisasa, kuleta kazi za huduma, na mara kwa mara kuweka maofisa wa vyeo mbali mbali kuendesha kijiji hicho. Mahala pengine tuliwashawishi vijana waondoke mjini waende katika sehemu fulani ya shamba, halafu tukawa-acha wajitegemee. Tulifanya mambo hayo kwa sababu tulitambua kwamba ardhi ni kitu muhimu kwa uchumi wetu wa baadaye, lakini tulipokuwa tukifanya hivyo tulidhani kuwa kuna njia ya

mkato ya kuendeleza sehemu hizo. Kwa hiyo mara kwa mara tuliwashawishi watu waende katika makazi mapya, tukiwaahidi kuwa wakienda huko watatajirika haraka haraka, au kuwa watapata huduma na vifaa ambavyo wasingeliweza kuvipata ama mjini ama vitongojini kwao. Mara chache sana tulieleza shabaha nyingine; mawazo na maneno yetu yote yalikuwa juu ya kutajirisha watu, na vifaa watakavyopata wale waendao katika makazi mpya.

Kwa kweli tulichokuwa tunafanya ni kufikiria maendeleo ya vitu, si ya watu. Kadhalika, tulifikiria wao kutumia mapesa ili kupata uchumi tuliokuwa tunautarajia. Yaani tulisema kuwa vifaa au fedha vitatuongezea uchumi, na mali hiyo itaweza kubadili maisha ya watu wanaohusika. Kitu cha kwanza tulichofikiria ni uchumi; halafu ndiyo watu. Kwa sababu hiyo kuna sehemu nyingi ambapo fedha nyingi zilizotumika hazikuleta maongezeko ya uchumi na hivyo fedha hizo zimepotea. Na karibu katika makazi mapya yote yaliyoanzishwa au kusaidiwa na Serikali, wengi katika wale waliokwenda katika makazi walivunjika moyo wakaondoka, au wameshindwa kufuata amri za wakubwa waliowekwa ambao kwa kweli si wakazi wa kijiji hicho na wala hawajali sana kufanikiwa au kushindwa kwa makazi hayo.

Kwa hiyo ni jambo muhimu kutambua kwamba siasa ya Ujamaa Vijijini shabaha yake siyo kufufua kwa jina jingine utaratibu wa zamani wa makazi mapya. Vijiji vya Ujamaa ni wazo jipya, na msingi wake ni kutambua, baada ya Azimio la Arusha, kwamba tunahitaji kuendeleza watu, siyo vitu; na kwamba watu wanaweza kujiendeleza wenyewe tu. Kwa kweli siasa hiyo ni matokeo ya kujifunza kutokana na makosa tuliyokwisha yafanya, na mafanikio ya vile vijiji vichache vilivyoanza na kukua kwa njia nyingine.

Vijiji vya Ujamaa vinatarajiwa viwe vijiji ambapyo vimeundwa na watu wenyewe, vikiendeshwa kijamaa na wale wanaoishi na kufanya kazi humo. Haviwezi kuundwa kutoka nje, wala kuendeshwa kutoka nje. Mtu hawezi kulazimishwa kuingia katika kijiji cha ujamaa, na kiongozi ye yote, wa kijijini au wa Serikali, hawezi kwenda akawaamrisha watu wanaokaa katika kijiji cha ujamaa wafanye nini kwa pamoja, na nini kila mtu peke yake. Hakuna Mkuu wa Serikali au wa TANU anayeweza kwenda katika kijiji cha Ujamaa na kuwaambia watu wapande mazao gani. Mtu

asiyekuwa wa kijiji kile hawezi kwenda akawaambia wakazi wa kijiji hicho watumie trekta, au wasitumie trekta. Maana mambo hayo yakitokea, yaani kama mtu wa nje anatoa amri na ana hakikisha kamba amri zinafuatwa, basi kijiji hicho hakiwi kijiji cha ujamaa tena.

Katika kijiji cha ujamaa watu huunganika kwa hiyari zao, wakaamua, kwa radhi yao wenyewe, kuishi pamoja na kufanya kazi pamoja kwa faida yao wote. Wao wenyewe wataamua shamba kiasi gani wataanza kulima pamoja, na shamba kiasi gani la mtu atalima peke yke; hakuna mtu mwingine anayeweza kuwafanyia uamuzi huo. Wao ndio wanaoweza kuamua jinsi ya kuzitumia fedha watakazozipata kwa shughuli za pamoja, kama kununua jembe la ng'ombe au kuleta maji, au kufanyia kazi nyingine. Hakuna mtu mwingine anayeweza kuwafanyia uamuzi huo. Wao, wao peke yao, ndiyo wataamua utaratibu wao wa kuishi na kufanya kazi.

Ni jambo muhimu mambo haya yaeleweke barabara. Ni muhimu pia kukumbuka kuwa watu wasishawishiwe kuanza kijiji cha ujamaa kwa ahadi za vitu watakavyovipewa wakienda huko. Watu waamue kuanzisha kijiji cha ujamaa kwa sababu wameelewa kwamba hivyo ndiyo njia peke yake kwao kuishi na kujiendeleza katika heshima na uhuru, wakivuna matunda yote ya shughuli zao za pamoja. Lazima waelewe kwamba yatakuwapo magumu na kwamba kuishi pamoja peke yake hakutawaletea maendeleo. Lazima waelewe kwamba kuishi kwao pamoja kunawezesha juhudi yao izae matunda bora zaidi hatimaye; lakini si kusema kwamba kuishi pamoja kutawapunguzia kazi.

Siasa ya Ujamaa Vijijini isipoeleweka japo kidogo na watu toka mwanzo watu wa kijiji hicho hawataweza kuvumilia shida za mwanzo. Maana hakuna aliye na hakika kwamba hakutakuwa na upungufu wa mazao katika mwaka wa kwanza au wa pili, au kama hakutatokea kiangazi kibaya, au mafuriko. Na amri ambazo ni ngumu zaidi za kijiji zitafuatwa vema ikiwa tu watu wanaelewa wanachofanya, na kwa sababu gani. Lakini kama shabaha na matumaini ya Vijiji vya Ujamaa yanaeleweka na kukubalika, basi watu wataweza kuyakabili matatizo hayo, na pengine watayatumia kuimarisha nia yao na kijiji chao. Matatizo yataharakisha maendeleo yao kuelekea ujamaa kamili. Lakini kwanza watu

lazima wafahamu kuwa kuishi kijamaa hakutendi miujiza kunawasaidia tu kuinua hali ya maisha yao.

Lakini kusema kuwa watu hawawezi kulazimishwa kwenda katika vijiji vya ujamaa, wala hawawezi kuambiwa jinsi ya kuviendesha, maana yake siyo kusema kwamba viongozi wa TANU na Serikali sasa wangoje tu wakitegemea kwamba watu wenyewe watapata moyo siku moja kuunda vijiji vya ujamaa. Ili vijiji vya ujamaa vianzishwe, na visaidiwe kustawi, watu lazima waelezwe, waelewe, na waongozwe. Hivyo ndivyo vitu ambavyo TANU inahitajiwa kufanya. Ni kazi yetu kueleza kijiji cha ujamaa ni kitu gani, na kuendelea kueleza mpaka watu wameelewa. Lakini uamuzi wa kuanzisha kijiji lazima uwe uamuzi wa watu wenyewe, na lazima kila mmoja aufanye uamuzi huo yeye mwenyewe binafsi. Maana kama watu 20 wamezungumza habari, hizo na 7 tu ndiyo waliokubaliana kuanzisha kijiji, basi kijiji hicho kitaanza kikiwa na watu 7. Kama 15 ndiyo walioamua kuanzisha, basi kitakuwa kijiji cha watu 15, na wengine watajiunga baadaye watakapokuwa tayari. Hakuna njia nyingine ya kuanzia, maana mtu akiamua kwenda katika kijiji cha ujamaa anaamua kuishi maisha ya aina fulani, na wale 5 wakija bila kuwa radhi wanaweza kuharibu juhudi ya wale wote 15 ambao wameamua kujiundia maisha mapya.

Uamuzi wa kuunganika na wengine katika kuunda kijiji cha ujamaa ni uamuzi wa kila mtu binafsi. Lakini uamuzi huo utakapokwisha kufanywa, basi utaratibu wa kawaida wa kuendesha mambo kidemokrasi hauna budi ufuatwe. Kwa mfano, wale watu 15 watakaa na kujadiliana kama inafaa kulima mashamba yao yote pamoja au kama wataanza kulima pamoja mazao ya kuuza tu, na kila mmoja ajilimie mwenyewe chakula. Wakiweza, watazungumza mpaka wakubaliane wote, lakini kama hawawezi kukubaliana wote kabla ya majira ya kulima kuanza, basi wataamua kwa kufuata maoni ya walio wengi. Uamuzi huo ukisha fanywa kabla ya majira ya kulima, basi wote lazima wakubali utaratibu wa kazi uliolazimika kuwekwa kwa mapenzi ya walio wengi, hata kama mtu binafsi alipinga uamuzi huo. Wakati wakifanya kazi kwa bidii, wale wachache wataendelea kujaribu kuwashawishi wenzao kubadili utaratibu mwakani, lakini maneno yao yasiwe ndiyo kisingizio cha kupinga au kupunguza juhudi wanayofanya katika kutimiza uamuzi ule.

Kwa kweli mara Kijiji cha Ujamaa kikisha undwa, demokrasi inafanya kazi. Maana kijiji cha ujamaa kinaonyesha mfano mzuri wa majadiliano ya watu walio sawa, mpaka wafikie uamuzi wa mambo yao wenyewe; kinaonyesha kwamba kama lazima mazungumzo yaachwe, na kazi ianze basi mawazo ya walio wengi ndiyo yatakayokubaliwa. Kijiji cha Ujamaa kinaonyesha haja ya watu kufuata utii na utaratibu wakati wa kutimiza uamuzi ambao wenyewe wanaufanya. Na katika njia hiyo hiyo watu wataanza kujiendeleza wenyewe kuwa watu wanaoheshimika na wanaojiamini wenyewe, hali ambayo hawawezi kuifikia kama wanafuata tu amri kutoka kwa mtu mwingine. Na hata kama "amri" za mtaalamu kama zikifuatwa bara bara zitasaidia kuongeza sana mazao hazibadili jambo hili. Kama jambo hili wamelizungumza na kuliamua wenyewe, watu hao watakuwa wamejiletea maendeleo. Maongezeko ya mapato yatakuja baadaye, wakati watakapokuwa wamejifunza kutoka mazoezi yao wenyewe, na wakati watakapoona wenyewe kwamba litakuwa jambo jema kujaribu maarifa mengine. Pengine maendeleo yataonekana kuwa ya pole pole kwa vile ambavyo mazao haya yataongezeka sana mwanzo. Lakini lazima tukumbuke kwamba wale waliotembea maili mia nyingi kuunga mkono Azimio la Arusha hawakuwa ni mabingwa wa kutembea haraka zaidi kuliko watu wengine. Walitembea pole pole kwa mwendo na saa zilizowafaa, mpaka wakatimiza lengo lao.

Lakini viongozi wa TANU na wa Serikali wanaweza kuvisaidia Vijiji vya Ujamaa na wale wanaoishi humo; na wanapaswa kufanya hivyo. Viongozi wanatakiwa wawasaidie watu kuelewa mambo yote mazuri na mabaya kuhusu njia mbali mbali za kufanya kazi. Ni vema tukikisaidia kikundi kilichoamua kuanzisha kijiji cha ujamaa kwa kuhakikisha kwamba wanapata ardhi ya kutosha katika sehemu inayofaa. Lazima tuwasaidie katika kueleza faida za kulima pamoja, na jinsi ya kumaliza matatizo yake. Tunapaswa kuhakikisha kwamba wataalam wako wa kutosha kuwashauri watu hao katika kazi za kilimo na kutoa mashauri ya kuwasaidia kufanya uamuzi wao.

Kadhalika viongozi wa TANU na wa Serikali lazima wahakikishe kwamba vijiji vya ujamaa vinafikiriwa kwanza katika kupata huduma zitakazoanza kusaidia juhudi na uamuzi wao. Kwa mfano, kama wananchi katika kijiji cha ujamaa wanaamua kwa-

mba shida yao kubwa ni maji, na kwamba wanaweza kuchimba mifereji na kununua bomba lakini hawana nguvu ya kununua mashine ya kusukumia maji, basi TANU na Serikali lazima iwasaidie hawa kupata mashine, kuliko kuweka mabomba mahala pengine. Lakini kusema hivyo si kusema kwamba msaada wa Serikali utumike badala ya juhudi za wananchi katika kijiji cha ujamaa. Mashauri na yatolewe; lakini uamuzi lazima uwe wa wale wale wanaoishi kijijini. Msaada lazima utolewe, lakini lakini msaada wenyewe uwe wa kusaidia kazi ambayo wananchi wenyewe wamekwisha ianza. Vijiji hivi lazima vianzishwe, na vikue, kwa kufuata msingi wa kujitegemea. Maana kujitegemea ndiyo njia ambayo watu watumia kujiendeleza.

Tanzania ni watu wote

Tukiwasaidia watu wa Tanzania kuendelea, ndiyo tunaendeleza Tanzania. Maana Tanzania ni ya Watanzania, na Watanzania ni wote. Hakuna mtu mwenye haki ya kusema, "Mimi ndiyo watu". Wala hakuna Mtanzania, mwenye haki ya kusema "Najua linalowafaa Watanzania, na wengine lazima wafuate."

Watanzania wote lazima waamue mambo ya Tanzania. Wote lazima wafanye kazi pamoja na wote sisi lazima tuzikubali kanuni tunazojiwekea. Lazima ziwe kanuni zetu wote, na wote tupaswe kuzifuata. Lakini katika kuzikubali kanuni hizo lazima tubaki watu huru, tunatimiza kanuni zetu wenyewe. Idadi ya watu wanaohusika na kila kanuni itatofautiana. Kanuni nyingine ni za taifa zima, na kanuni ya namna hiyo ndiyo sheria ambayo wote tunapaswa kuitii. Kanuni nyingine zinawahusu wale wanaoishi katika mji fulani, au Wilaya fulani, na hizo huitwa sheria ndogo. Zingine zinatokana na uamuzi wetu wenyewe kushiriki katika kikundi fulani: kufanya kazi katika kiwanda, kuishi katika kijiji cha ujamaa, n.k.; na utii unatuhusu kwa sababu tumekuwa wanachama wa kikundi hicho. Lakini Watanzania ni sisi wote. Wananchi ni sisi wote kwa pamoja. Maendeleo ni yetu na ni juu yetu wenyewe; na maendeleo tunayoyataka ni maendeleo ya watu: yaletwe na watu; yaendeleze watu; yawafae watu.

Kimepigwa Chapa na: CUT PRESS, S.L.P. 2567, Dar es Salaam